JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FUNGU 80

MKOA WA MTWARA

MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/17, NUSU MWAKA 2017/18 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2018/2019 KWA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 544,
MTWARA
Simu/Nukushi: 023 – 2333194
Barua pepe: rc@mtwara.go.tz/ras@mtwara.go.tz
Tovuti: www.mtwara.go.tz

Machi, 2018

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari utekelezaji wa bajeti ya fungu 80-Mkoa wa Mtwara ikijumuisha Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2016/2017, nusu mwaka 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019. Aidha, utekelezaji wa bajeti ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/17-2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (2015-2020), Mipango mikakati ya Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Hotuba ya Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuzindua Bunge la 11 na mipango mbalimbali ya kisekta.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2018/2019, Mkoa umejiwekea vipaumbele katika maeneo yafuatayo;

- Uboreshaji wa miundombinu katika shule za msingi.
- Uboreshaji wa miundombinu katika shule za sekondari.
- Uboreshaji wa miundombinu ya afya (hospitali, zahanati na vituo vya afya).
- Uboreshaji wa huduma za kilimo.
- Uandaaji wa mazingira wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.
- Uboreshaji wa miundombinu ya maji.
- Uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

2.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI

2.1.1 Makadirio na Makusanyo ya Sekretarieti ya Mkoa kwa mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi **541,000.00** kutoka chanzo cha kodi ya pango katika nyumba tano za Serikali kama mapato ya Serikali yanayokwenda moja kwa moja Hazina. Hadi Juni, 2017 jumla ya shilingi **1,062,000.00** zilikusanywa sawa na asilimia **196.30** ya makadirio. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezwa kwa viwango vya pango baada ya bajeti kupitishwa.

2.1.2 Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Halmashauri zilikadiria kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi **25,171,728,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi Juni, 2017 jumla ya shilingi **24,932,667,000.00** zilikusanywa sawa na **99.05%** ya makadirio. Jedwali Na.1 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.1: Makadirio na Makusanyo ya Mapato ya Ndani Halmashauri hadi Juni, 2017

HALMASHAURI	MAKADIRIO 2016/17	MAKUSANYO HADI JUNI, 2017			
		MAKUSANYO YASIYOLINDWA	MAKUSANYO LINDWA	JUMLA	%
Mtwara Mikindani	4,542,968,000	3,505,908,000	276,839,000	3,782,747,000	**83.27**
Masasi Mji	1,867,104,000	1,587,375,000	376,046,000	1,963,421,000	**105.16**
Newala Mji	1,939,486,000	1,505,497,000	486,886,000	1,992,383,000	**102.73**
Nanyamba Mji	1,226,868,000	1,352,700,000	44,571,000	1,397,271,000	**113.89**
Mtwara	2,306,244,000	1,539,884,000	182,123,000	1,722,007,000	**74.67**
Masasi	4,003,191,000	2,320,642,000	1,560,993,000	3,881,635,000	**96.96**
Nanyumbu	2,407,389,000	1,783,651,000	681,203,000	2,464,854,000	**102.39**
Newala	1,996,264,000	1,223,342,000	415,313,000	1,638,655,000	**82.09**
Tandahimba	4,882,214,000	4,842,065,000	1,247,629,000	6,089,694,000	**124.73**
JUMLA	**25,171,728,000**	**19,661,064,000**	**5,271,603,000**	**24,932,667,000**	**99.05**

Tanbihi: *Makusanyo lindwa ni mapato yanayojumuisha vyanzo vya ada ya huduma (user fee), mfuko wa afya ya jamii (CHF), mfuko wa elimu na export levy. Matumizi ya fedha hizi huzingatia sheria ya CHF, Mfuko wa elimu na miongozo ya matumizi ya ada ya huduma na export levy.*

Sababu za baadhi ya Halmashauri kutofikia malengo ya makusanyo ni;

- Kushuka kwa bei za mazao mchanganyiko mfano mbaazi.
- Kurejeshwa kiasi kidogo cha kodi ya majengo.
- Kutorejeshwa kwa 30% ya kodi ya ardhi kutoka Wizara ya Ardhi.

Aidha, Halmashauri zilizovuka lengo ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la korosho na hivyo ushuru wa zao la korosho kuongezeka zaidi ya makadirio yaliyofanyika wakati wa kuandaa bajeti.

Matumizi ya mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kwa makusanyo yasiyolindwa ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba 2. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa zimeoneshwa katika ukurasa wa 8 na 9.

Jedwali Na.2: Matumizi ya makusanyo yasiyolindwa kwa mwaka 2016/2017

HALMASHAURI	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	Wanawake na Vijana (10%)				Miradi ya Maendeleo (50%)			
		Takiwa	%	Tengwa	%	Takiwa	%	Tengwa	%
Mtwara Mikind	3,505,908,000	350,590,800	10	350,590,800	**10.00**	1,752,954,000	50	1,760,833,759	**50.22**
Masasi Mji	1,587,375,000	158,737,500	10	149,109,000	**9.39**	793,687,500	50	686,459,354	**43.24**
Newala Mji	1,505,497,000	150,549,700	10	144,366,000	**9.59**	752,748,500	50	818,238,167	**54.35**
Nanyamba Mji	1,352,700,000	135,270,000	10	104,725,000	**7.74**	676,350,000	50	589,823,528	**43.60**
Mtwara	1,539,884,000	153,988,400	10	95,723,000	**6.22**	769,942,000	50	489,635,432	**31.80**
Masasi	2,320,642,000	232,064,200	10	217,845,600	**9.39**	1,089,228,000	50	683,451,311	**29.45**
Nanyumbu	1,783,651,000	178,365,100	10	178,365,100	**10.00**	891,825,500	50	955,135,443	**53.55**
Newala	1,223,342,000	122,334,200	10	130,000,000	**10.63**	611,671,000	50	479,479,364	**39.19**
Tandahimba	4,842,065,000	484,206,500	10	316,800,000	**6.54**	2,421,032,500	50	3,154,292,181	**65.14**
JUMLA	**19,661,064,000**	**1,966,106,400**	**10**	**1,687,524,500**	**8.58**	**9,759,439,000**	**50**	**9,617,348,539**	**48.92**

Nyongeza: Orodha ya vikundi vilivyokopeshwa vimeoneshwa katika kiambatisho namba 1 kwenye randama.

2.2 FEDHA ZA RUZUKU KWA *MATUMIZI YA KAWAIDA* MWAKA 2016/2017

2.2.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishwa jumla ya shilingi **6,930,724,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Juni, 2017 ni jumla ya shilingi **6,344,005,000.00** sawa na **91.53%** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **6,344,005,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizotolewa. Jedwali na.3 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.3: Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Juni, 2017

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Mishahara	5,372,873,000	4,793,847,000	89.22	4,793,847,000	**100.00**
Matumizi Mengineyo	1,557,851,000	1,550,158,000	99.51	1,550,158,000	**100.00**
JUMLA	**6,930,724,000**	**6,344,005,000**	**91.53**	**6,344,005,000**	**100.00**

Tanbihi: *Pamoja na fedha hizo, Sekretarieti ya Mkoa ilipokea jumla ya sh.* ***556,490,000*** *kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali ikiwa madeni ya wazabuni sh.* ***100,793,000*** *na madeni ya watumishi sh.* ***455,697,000****.*

2.2.2 Shughuli zilizotekelezwa hadi Juni, 2017

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa hadi Juni, 2017 kwa fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na;

- Kusimamia ulinzi na usalama ndani ya Mkoa.
- Kuendesha vikao tisa (9) vya kisheria (RCC, DCC na Road Board).
- Kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali za kila siku za kutoa huduma kwa wananchi na kutoa ushauri kwa Halmashauri.

- Kulipa mishahara kwa watumishi 528.
- Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa Mkoa na kitaifa.
- Kuratibu ukimbizaji wa mbio za mwenge wa uhuru.
- Kutoa huduma za tiba na kinga katika hospitali ya Mkoa.

2.2.3 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2016/17

Katika mwaka 2016/17 Halmashauri ziliidhinishiwa fedha za ruzuku jumla ya shilingi **122,660,965,628.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Juni, 2017 ni jumla ya shilingi **119,136,810,294.00** sawa na asilimia **97.20**. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **119,136,810,294.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.4 na 5 yanaonesha michanganuo yake.

Jedwali Na.4: Bajeti na Mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Juni, 2017

HALMASHAURI	BAJETI		FEDHA TOLEWA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	13,153,215,000	1,748,196,704	12,705,817,900	**96.60**	1,748,196,704	**100.00**
Masasi Mji	11,384,584,000	1,104,861,000	10,942,273,300	**96.11**	1,023,643,261	**92.70**
Newala Mji	*	723,213,000	160,706,000	**na**	671,448,305	**92.90**
Nanyamba Mji	*	753,273,302	5,959,026,500	**na**	753,273,302	**100.00**
Mtwara	18,827,274,000	1,282,396,094	12,238,255,500	**65.00**	1,282,396,094	**100.00**
Masasi	17,886,733,000	2,513,666,513	17,653,530,400	**98.70**	2,513,666,513	**100.00**
Nanyumbu	12,055,444,000	956,760,603	12,055,444,800	**100.00**	956,760,603	**100.00**
Newala	18,391,530,000	848,429,576	17,311,980,100	**94.13**	848,429,576	**100.00**
Tandahimba	19,536,773,000	1,494,615,836	18,817,345,600	**96.32**	1,494,615,836	**100.00**
JUMLA	**111,235,553,000**	**11,425,412,628**	**107,844,380,100**	**99.37**	**11,292,430,194**	**98.90**
JUMLA KUU	**122,660,965,628**		**119,136,810,294**			**97.20**

***** *Halmashauri hizi zilianzishwa rasmi tarehe 01/07/2015. Hivyo, kwa mwaka 2016/17 bajeti ya mishahara ilikasimiwa katika Halmashauri mama*.

Jedwali Na.5: Fedha zilizotolewa na kutumika kwa Matumizi ya kawaida hadi Juni, 2017

HALMASHAURI	FEDHA ZILIZOTOLEWA		FEDHA ZILIZOTUMIKA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	12,705,817,900	1,748,196,704	12,705,817,900	**100**	1,748,196,704	**100**
Masasi Mji	10,942,273,300	1,023,643,261	10,942,273,300	**100**	1,023,643,261	**100**
Newala Mji	160,706,000	671,448,305	160,706,000	**100**	671,448,305	**100**
Nanyamba Mji	5,959,026,500	753,273,302	5,959,026,500	**100**	753,273,302	**100**
Mtwara	12,238,255,500	1,282,396,094	12,238,255,500	**100**	1,282,396,094	**100**
Masasi	17,653,530,400	2,513,666,513	17,653,530,400	**100**	2,513,666,513	**100**
Nanyumbu	12,055,444,800	956,760,603	12,055,444,800	**100**	956,760,603	**100**
Newala	17,311,980,100	848,429,576	17,311,980,100	**100**	848,429,576	**100**
Tandahimba	18,817,345,600	1,494,615,836	18,817,345,600	**100**	1,494,615,836	**100**
JUMLA	**107,844,380,100**	**11,292,430,194**	**107,844,380,100**	**100**	**11,292,430,194**	**100**
JUMLA KUU	**119,136,810,294**		**119,136,810,294**			**100**

2.2.4 Shughuli zilizotekelezwa hadi Juni, 2017

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Juni, 2017 kwa fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na;

- Kulipa mishahara ya watumishi kwa Halmashauri tisa (9).
- Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli zilizotekelezwa katika Kata,Vijiji/Mitaa na Vitongoji.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.
- Uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Kuratibu utoaji wa elimu bila malipo.
- Mbio za mwenge wa Uhuru.

2.3 FEDHA ZA RUZUKU KWA *MIRADI YA MAENDELEO* MWAKA 2016/2017

2.3.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2016/17

Katika mwaka wa fedha 2016/17 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishiwa jumla ya shilingi **1,577,566,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **1,110,000,000.00 (70.36%)** ni fedha za ndani na shilingi **467,566,000.00 (29.64%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Juni, 2017 jumla ya shilingi **701,844,000.00** zilitolewa sawa na asilimia **44.49**. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **701,844,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.6 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.6. Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Juni, 2017

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Fedha za Ndani	1,110,000,000	270,000,000	24.32	270,000,000	100.00
Fedha za Nje	467,566,000	431,844,000	92.36	431,844,000	100.00
JUMLA	**1,577,566,000**	**701,844,000**	**44.49**	**701,844,000**	**100.00**

2.3.2 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Juni, 2017

Orodha ya baadhi ya Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa hadi Juni, 2017 ni pamoja na;

- Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu za maji, mfuko wa pamoja wa sekta ya afya na miradi ya maendeleo katika Halmashauri.
- Kufanya utekelezaji wa programu ya maboresho ya menejimenti ya fedha za umma (PFMRP IV).
- Kufanya maboresho ya ukumbi wa mikutano katika jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

2.3.3 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2016/17

Katika mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ziliidhinishiwa jumla ya shilingi **19,948,568,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **11,288,344,000.00 (56.60%)** ni fedha za ndani na shilingi **8,660,224,000.00 (43.40%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Juni, 2017 jumla ya shilingi **8,977,593,824.00** zilitolewa sawa na **45.00%.** Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **5,977,784,824.00** sawa na **66.59%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.7 na 8 yanaonesha michanganuo yake.

Jedwali Na.7: Bajeti na Fedha za ruzuku ya miradi zilizotolewa hadi Juni, 2017

HALMASHAURI	BAJETI IDHINISHWA		FEDHA TOLEWA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	570,526,000	3,349,663,000	183,645,000	**32.19**	235,731,378	**7.04**
Masasi Mji	1,284,760,000	719,561,000	926,599,000	**72.12**	269,809,791	**37.50**
Newala Mji	2,487,749,000	111,619,000	1,103,739,000	**44.37**	111,619,000	**100.00**
Nanyamba Mji	2,556,219,000	366,832,000	1,131,194,000	**44.25**	302,332,000	**82.42**
Mtwara	1,271,703,000	526,370,000	958,763,000	**75.39**	341,853,204	**64.95**
Masasi	1,111,686,000	888,617,000	375,945,000	**33.82**	634,331,049	**71.38**
Nanyumbu	584,281,000	739,826,000	230,281,000	**39.41**	739,826,000	**100.00**
Newala	455,578,000	595,576,000	184,569,000	**40.51**	372,325,916	**62.52**
Tandahimba	965,842,000	1,362,160,000	329,590,000	**34.12**	545,440,486	**40.04**
JUMLA	**11,288,344,000**	**8,660,224,000**	**5,424,325,000**	**48.05**	**3,553,268,824**	**41.10**
JUMLA KUU	**19,948,568,000**		**8,977,593,824**			**45.00**

Jedwali Na.8: Fedha za ruzuku ya miradi zilitolewa na zilizotumika hadi Juni, 2017

HALMASHAURI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	183,645,000	235,731,378	157,987,580	**86.03**	235,731,378	**100.00**
Masasi Mji	926,599,000	269,809,791	176,580,000	**19.06**	238,414,000	**88.36**
Newala Mji	1,103,739,000	111,619,000	297,874,000	**26.99**	111,619,000	**100.00**
Nanyamba Mji	1,131,194,000	302,332,000	625,329,000	**55.28**	206,116,201	**68.18**
Mtwara	958,763,000	341,853,204	329,936,000	**34.41**	341,812,361	**99.99**
Masasi	375,945,000	634,331,049	368,106,000	**97.91**	628,546,957	**99.09**
Nanyumbu	230,281,000	739,826,000	205,789,557	**89.36**	629,571,388	**85.10**
Newala	184,569,000	372,325,916	184,569,000	**100.00**	364,771,916	**99.00**
Tandahimba	329,590,000	545,440,486	329,590,000	**100.00**	545,440,486	**100.00**
JUMLA	**5,424,325,000**	**3,553,268,824**	**2,675,761,137**	**49.33**	**3,302,023,687**	**92.93**
JUMLA KUU	**8,977,593,824**		**5,977,784,824**			**66.59**

Pamoja na fedha hizo, Halmashauri zilipokea na kutumia fedha za TASAF kama inavyooneshwa katika jedwali namba 9.

Jedwali Na.9: Fedha za TASAF zilizitolewa na kutumika 2016/17

HALMASHAURI	TASAF		
	Tolewa	**Tumika**	**%**
Mtwara Mikindani	449,984,000	446,572,000	**99.24**
Masasi Mji	644,355,000	623,573,000	**96.77**
Newala Mji	*		
Nanyamba Mji	*		
Mtwara	2,046,602,520	2,003,102,300	**97.87**
Masasi	2,848,141,000	2,490,286,000	**87.44**
Nanyumbu	2,014,668,000	1,931,073,000	**95.85**
Newala	1,622,983,000	1,507,983,000	**92.91**
Tandahimba	1,650,316,000	1,650,316,000	**100.00**
JUMLA	**11,277,049,520**	**10,652,905,300**	**94.47**

***Fedha za Halmashauri hizi zinapitia Halmashauri mama.*

2.3.4 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Juni, 2017.

Orodha ya baadhi ya Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Juni, 2017 ni pamoja na;

- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 151 kwa shule za msingi.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 60 kwa shule za sekondari.
- Ujenzi wa nyumba za watumishi 48 (walimu na watumishi wa afya).
- Ujenzi wa zahanati 20.
- Ujenzi wa vituo vya afya 4.
- Ujenzi wa ofisi za vijiji 11 na ujenzi wa ofisi za kata 15.
- Ujenzi wa miradi ya maji 6.
- Utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kaya 44,760 zilizopo katika vijiji/mitaa 512.
- Ujenzi wa majengo manne (4) ya utawala kwa Halmashauri za Newala Mji, Nanyamba Mji, Masasi Mji na Masasi.

- Kupima maeneo 159 vya taasisi za Serikali.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 465 kwa shule za msingi.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 119 kwa shule za sekondari.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18 KWA KIPINDI CHA JULAI HADI FEBRUARI, 2018.

3.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI MWAKA 2017/18

3.1.1 Makadirio na Makusanyo ya Sekretarieti ya Mkoa kwa mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi **4,400,000.00** kutoka chanzo cha kodi ya ukumbi, mgahawa na mauzo ya nyaraka za zabuni kama mapato ya Serikali yanayokwenda moja kwa moja Hazina. Hadi Februari, 2018 jumla ya shilingi **600,000.00** zimekusanywa sawa na **13.70%** ya makadirio. Makusanyo yako chini ya wastani kutokana na pango la mgahawa kutarajiwa kulipwa mwezi Mei, 2018 na nyaraka za zabuni hazijauzwa kutokana na fedha za miradi yenye zabuni kutotolewa ili kuwezesha utekelezaji.

3.1.2 Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi **30,333,661,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi Februari, 2018 jumla ya shilingi **19,695,135,000.00** zimekusanywa sawa na **64.93%** ya lengo. Jedwali Na.10 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.10: Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	MAKADIRIO	MAKUSANYO HADI FEB, 2017			
		MAKUSANYO YASIYOLINDWA	MAKUSANYO LINDWA	JUMLA	%
Mtwara Mikindani	5,681,867,000	3,489,649,000	487,582,000	3,977,231,000	**69.99**
Masasi Mji	2,708,564,000	1,067,919,000	455,743,000	1,523,662,000	**56.25**
Newala Mji	2,216,082,000	929,295,000	449,869,000	1,379,164,000	**62.23**
Nanyamba Mji	2,115,930,000	946,445,000	379,666,000	1,326,111,000	**62.67**
Mtwara	2,623,495,000	1,409,340,000	130,697,000	1,540,037,000	**58.70**
Masasi	4,169,626,000	1,467,550,000	481,554,000	1,949,104,000	**46.80**
Nanyumbu	2,941,967,000	1,112,573,000	774,214,000	1,886,787,000	**64.13**
Newala	2,062,662,000	840,364,000	387,044,000	1,227,408,000	**59.51**
Tandahimba	5,813,468,000	3,366,318,000	1,519,313,000	4,885,631,000	**84.04**
JUMLA	**30,333,661,000**	**14,629,453,000**	**5,065,682,000**	**19,695,135,000**	**64.93**

Tanbihi: *Makusanyo lindwa ni mapato yanayojumuisha vyanzo vya ada ya huduma (user fee), mfuko wa afya ya jamii (CHF) na mfuko wa elimu. Matumizi ya fedha hizi huzingatia sheria CHF, Mfuko wa elimu na miongozo ya ada ya huduma.*

Halmashauri hazikuweza kufikia wastani wa malengo ya makusanyo kwa kipindi cha nusu mwaka kutokana na;

- Kushuka kwa soko la zao la mbaazi.
- Mavuno kwa mazao mchanganyiko kuanza mwezi April, 2018.
- Mabadiliko ya sheria ya ushuru wa mazao yaliyopelekea kupunguzwa kwa kiwango cha ushuru wa mazao kutoka 5% hadi 3%.
- Kuondolewa kwa chanzo cha export levy.
- Kushuka kwa bei za mazao mchanganyiko kama ufuta na choroko.
- Maelekezo ya Serikali kuacha kukusanya ushuru kwa usafirshaji wa mazao chini tani moja.

Matumizi ya mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kwa makusanyo yasiyolindwa ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba 11 ambapo jumla ya sh. **1,284,709,000.00 (8.78%)** za wanawake, vijana na walemavu zimetengwa kati ya sh. **14,629,453,000.00.** Miradi mingine ya maendeleo jumla ya sh. **6,809,817,000.00 (46.55%)** zimetengwa kati ya sh. **14,629,453,000.00**.

Jedwali Na.11: Matumizi ya makusanyo yasiyolindwa hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	Wanawake, Vijana na Walemavu (10%)				Miradi ya Maendeleo (50%)			
		Takiwa	%	Tengwa	%	Takiwa	%	Tengwa	%
Mtwara Mikindani	3,489,649,000	348,965,000	10	325,000,000	**9.31**	1,744,825,000	50	1,744,825,000	**50.00**
Masasi Mji	1,067,919,000	106,792,000	10	90,000,000	**8.43**	533,959,000	50	387,511,000	**36.29**
Newala Mji	929,295,000	92,929,000	10	92,929,000	**10.0**	464,647,000	50	464,647,000	**50.00**
Nanyamba Mji	946,445,000	94,644,000	10	87,000,000	**9.19**	473,222,000	50	433,000,000	**45.75**
Mtwara	1,409,340,000	140,934,000	10	88,318,000	**6.27**	704,670,000	50	370,673,000	**26.30**
Masasi	1,467,550,000	146,755,000	10	105,620,000	**7.20**	733,775,000	50	392,000,000	**26.80**
Nanyumbu	1,112,573,000	111,257,000	10	79,210,000	**7.12**	556,286,000	50	577,370,000	**51.89**
Newala	840,364,000	84,036,000	10	80,000,000	**9.52**	420,182,000	50	420,000,000	**49.98**
Tandahimba	3,366,318,000	336,632,000	10	336,632,000	**10.0**	1,683,159,000	50	2,019,791,000	**60.00**
JUMLA	**14,629,453,000**	**1,462,944,000**	**10**	**1,284,709,000**	**8.78**	**7,314,725,000**	**50**	**6,809,817,000**	**46.55**

Tanbihi: Orodha ya vikundi vilivyokopeshwa vimeoneshwa katika kiambatisho namba 2 kwenye randama.

Aidha, baadhi ya shughuli zilizozotekelezwa zimeoneshwa katika ukurasa wa 18

3.2 FEDHA ZA RUZUKU KWA *MATUMIZI YA KAWAIDA* MWAKA 2017/2018

3.2.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Sekretarieti ya Mkoa iliidhinishwa jumla ya shilingi **7,178,976,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2018 ni jumla ya shilingi **4,135,824,000.00** sawa na **57.61%** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **4,135,824,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizotolewa. Jedwali Na.12 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.12: Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Feb, 2018

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Mishahara	5,514,656,000	3,125,323,000	56.67	3,125,323,000	100.00
Matumizi Mengineyo	1,664,320,000	1,010,501,000	60.72	1,010,501,000	100.00
JUMLA	**7,178,976,000**	**4,135,824,000**	**57.61**	**4,135,824,000**	**100.00**

3.2.2 Shughuli zilizotekelezwa hadi Februari, 2018

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa hadi Februari, 2018 kwa fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na;

- Kusimamia ulinzi na usalama ndani ya Mkoa.
- Kuendesha vikao vya vinne (4) vya kisheria.
- Kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali za kila siku za kutoa huduma kwa wananchi na kutoa ushauri kwa Halmashauri.
- Kulipa mishahara kwa watumishi kwa watumishi 416
- Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya elimu msingi na sekondari.
- Kuratibu ziara za viongozi mbalimbali wa Mkoa na kitaifa.
- Kutoa huduma za tiba na kinga katika hospitali ya Mkoa.

3.2.3 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya fedha za ruzuku zenye jumla ya shilingi **131,921,353,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili kugharamia maeneo ya mishahara na matumizi mengineyo. Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2018 ni jumla ya shilingi **74,441,173,000.00** sawa na **56.43%** ya makadirio. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **74,441,173,000.00** sawa na **100.00%** ya fedha zilizopokelewa Jedwali Na.13 na 14 yanaonesha michanganuo yake.

Jedwali Na.13: Bajeti na Mapokezi ya fedha za Matumizi ya Kawaida hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	BAJETI		FEDHA TOLEWA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	14,317,074,000	676,190,000	8,525,939,000	**59.55**	392,153,000	**57.99**
Masasi Mji	11,865,530,000	575,851,000	7,388,881,000	**62.27**	341,011,000	**59.22**
Newala Mji*	750,246,000	455,767,000	2,923,005,000	**na**	278,288,000	**61.06**
Nanyamba Mji	8,297,661,000	462,151,000	4,539,273,000	**54.71**	300,632,000	**65.05**
Mtwara	13,806,577,000	637,800,000	7,290,377,000	**52.80**	406,995,000	**63.81**
Masasi	19,264,953,000	1,043,086,000	11,599,728,000	**60.21**	668,077,000	**64.05**
Nanyumbu	15,873,225,000	735,964,000	7,661,640,000	**48.27**	470,275,000	**63.90**
Newala	20,692,932,000	848,015,000	8,470,652,000	**40.93**	526,996,000	**62.14**
Tandahimba	20,539,348,000	1,078,983,000	11,977,275,000	**58.31**	679,976,000	**63.02**
JUMLA	**125,407,546,000**	**6,513,807,000**	**70,376,770,000**	**56.12**	**4,064,403,000**	**62.40**
	131,921,353,000		**74,441,173,000**			**56.43**

*****Fedha za mishahara kwa Halmashauri ya Mji Newala zilizotolewa ni kubwa zaidi ya bajeti imetokana na wakati wa uandaaji wa bajeti watumishi wengi walikuwa hawajahamishwa kutoka Halmashauri mama ya Wilaya ya Newala.

Jedwali Na.14: Fedha zilizotolewa na kutumika kwa Matumizi ya kawaida hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	FEDHA ZILIZOTOLEWA		FEDHA ZILIZOTUMIKA			
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MISHAHARA	%	MATUMIZI MENGINEYO	%
Mtwara Mikindani	8,525,939,000	392,153,000	8,525,939,000	100	392,153,000	100
Masasi Mji	7,388,881,000	341,011,000	7,388,881,000	100	341,011,000	100
Newala Mji	2,923,005,000	278,288,000	2,923,005,000	100	278,288,000	100
Nanyamba Mji	4,539,273,000	300,632,000	4,539,273,000	100	300,632,000	100
Mtwara	7,290,377,000	406,995,000	7,290,377,000	100	406,995,000	100
Masasi	11,599,728,000	668,077,000	11,599,728,000	100	668,077,000	100
Nanyumbu	7,661,640,000	470,275,000	7,661,640,000	100	470,275,000	100
Newala	8,470,652,000	526,996,000	8,470,652,000	100	526,996,000	100
Tandahimba	11,977,275,000	679,976,000	11,977,275,000	100	679,976,000	100
JUMLA	**70,376,770,000**	**4,064,403,000**	**70,376,770,000**	**100**	**4,064,403,000**	**100**
	74,441,173,000		**74,441,173,000**			**100**

3.2.4 Shughuli zilizotekelezwa hadi Februari, 2018

Orodha ya baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Februari, 2018 kwa fedha za matumizi ya kawaida ni pamoja na;

- Kulipa mishahara kwa watumishi 11,629.

- Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli zilizotekelezwa katika Kata,Vijiji/Mitaa na Vitongoji.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi.
- Kuendesha vikao vya mbalimbali vya kisheria.

3.4 FEDHA ZA RUZUKU KWA *MIRADI YA MAENDELEO* MWAKA 2017/2018

3.4.1 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Sekretarieti ya Mkoa mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa jumla ya shilingi **1,699,150,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi **1,330,000,000.00 (78.27%)** ni fedha za ndani na shilingi **369,150,000.00 (21.73%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya shilingi **450,828,000.00** zimetolewa sawa na **26.53%** ya bajeti idhinishwa. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **286,050,000.00** sawa na **64.00%** ya fedha zilizopokelewa. Jedwali Na.15 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.15. Bajeti, Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Feb, 2018

KASMA	BAJETI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
		KIASI	%	KIASI	%
Fedha za Ndani	1,330,000,000	365,000,000	27.44	249,475,000	68.35
Fedha za Nje	369,150,000	85,828,000	23.25	36,575,000	42.61
JUMLA	**1,699,150,000**	**450,828,000**	**26.53**	**286,050,000**	**64.00**

3.4.2 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Februari, 2018.

Orodha ya baadhi ya program/miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Sekretarieti ya Mkoa hadi Februari, 2018 kwa fedha zilizotolewa ni;

- Kufuatilia utekelezaji wa programu ya maji katika Halmashauri zote.

- Kuratibu na kuwasilisha GPSA fedha za ununuzi wa gari la Mhe.Mkuu wa Mkoa.
- Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini katika Halmashauri zote.
- Ufuatiliaji wa miradi ya sekta ya elimu katika Halmashauri zilizopata fedha za P4R.

3.4.3 Fedha zilizoidhinishwa na kutolewa kwa Halmashauri 2017/18

Katika mwaka 2017/18 Halmashauri zimeidhinishiwa fedha za ruzuku jumla ya shilingi **32,888,351,000.00** ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **21,692,280,000.00 (66.00%)** ni fedha za ndani na shilingi **11,196,071,000.00 (34.00%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya shilingi **11,076,839,000.00** zimetolewa sawa na **33.69%** ya makadirio. Aidha, kiasi kilichotumika ni shilingi **4,532,009,576.00** sawa na **40.90%** ya fedha zilizopokelewa**.** Jedwali Na.16 na 17 yanaonesha michanganuo yake.

Jedwali Na.16. Bajeti na Fedha za ruzuku ya miradi zilizotolewa hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	BAJETI IDHINISHWA		FEDHA TOLEWA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	2,064,698,000	4,536,533,000	910,576,000	**44.10**	183,084,000	**4.03**
Masasi Mji*	2,293,931,000	577,058,000	996,206,000	**43.43**	577,058,000	**100.00**
Newala Mji	2,835,166,000	166,385,000	1,483,582,000	**52.33**	61,764,000	**37.12**
Nanyamba Mji	2,929,565,000	347,201,000	1,437,597,000	**49.07**	83,695,000	**24.11**
Mtwara	2,286,385,000	550,447,000	638,712,000	**27.94**	217,547,000	**39.52**
Masasi	3,752,900,000	958,227,000	1,802,428,000	**48.03**	288,795,000	**30.14**
Nanyumbu	1,656,071,000	563,923,000	450,802,000	**27.22**	235,432,000	**29.51**
Newala	1,503,175,000	587,351,000	423,573,000	**28.18**	192,998,000	**32.86**
Tandahimba	2,370,389,000	2,908,946,000	829,245,000	**34.98**	266,745,000	**9.17**
JUMLA	**21,692,280,000**	**11,196,071,000**	**8,972,721,000**	**41.36**	**2,107,118,000**	**18.90**
JUMLA KUU	**32,888,351,000**		**11,079,839,000**			**33.69**

*****Halmashauri ya Masasi Mji inaonekana imepokea fedha zote za nje kutokana na kupokea fedha za kulipa wakandarasi wa miradi ya maji waliofanya kazi mwaka uliopita.

Jedwali Na.17: Fedha za ruzuku ya miradi zilitolewa na zilizotumika hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA			
	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	%	FEDHA ZA NJE	%
Mtwara Mikindani	910,576,000	183,084,000	565,582,000	**62.11**	75,685,000	**41.34**
Masasi Mji	996,206,000	577,058,000	292,351,000	**29.35**	56,408,000	**9.78**
Newala Mji	1,483,582,000	61,764,000	236,092,000	**15.91**	9,119,000	**14.76**
Nanyamba Mji	1,437,597,000	83,695,000	281,562,000	**19.59**	67,330,000	**80.45**
Mtwara	638,712,000	217,547,000	388,622,000	**60.84**	101,808,000	**46.80**
Masasi	1,802,428,000	288,795,000	940,245,074	**5217**	238,435,916	**82.56**
Nanyumbu	450,802,000	235,432,000	329,059,236	**72.99**	92,864,000	**39.44**
Newala	423,573,000	192,998,000	276,000,000	**65.16**	101,711,000	**52.70**
Tandahimba	829,245,000	266,745,000	275,456,000	**33.22**	203,679,350	**76.36**
JUMLA	**8,972,721,000**	**2,107,118,000**	**3,584,969,310**	**39.95**	**947,040,266**	**44.94**
JUMLA KUU	**11,079,839,000**		**4,532,009,576**			**40.90**

Pamoja na fedha hizo Halmashauri zimepokea fedha za TASAF III na ujenzi wa vituo vya afya 7 kama inavyooneshwa katika jedwali namba 18.

Jedwali Na.18: Fedha za TASAF zilizitolewa na kutumika hadi Feb, 2018

HALMASHAURI	TASAF			VITUO VYA AFYA	VITUO
	Tolewa	Tumika	%		
Mtwara Mikindani	224,619,633	223,950,700	**99.70**	500,000,000	1
Masasi Mji	663,494,301	586,155,610	**88.34**		
Newala Mji	*				
Nanyamba Mji	*			1,400,000,000	3
Mtwara	1,018,450,360	1,018,450,360	**100.0**		
Masasi	1,977,858,751	1,967,858,751	**99.49**	400,000,000	1
Nanyumbu	1,579,066,574	1,300,012,089	**82.33**		
Newala	1,124,773,547	1,123,800,000	**99.91**	400,000,000	1
Tandahimba	1,678,562,510	1,675,402,423	**99.90**	400,000,000	1
JUMLA	**8,266,825,676**	**7,895,629,933**	**95.55**	**3,100,000,000**	**7**

***Fedha za Halmashauri hizi zinapitia Halmashauri mama.*

3.4.4 Program/Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa hadi Februari, 2018.

Orodha ya baadhi ya program/miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Februari, 2018 kwa fedha zilizotolewa ni pamoja na;

- Ujenzi wa miradi 20 ya maji.
- Ujenzi wa vituo vya afya 7.
- Utekelezaji wa shughuli za mfuko wa jimbo.
- Utekelezaji wa zoezi la uandikishaji na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano.
- Utoaji wa elimu bila malipo katika shule zote za msingi na sekondari.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 161 kwa shule za msingi.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 89 kwa shule za sekondari.
- Ujenzi wa majengo manne (4) ya utawala kwa Halmashauri za Newala Mji, Nanyamba Mji, Masasi Mji na Masasi.
- Ujenzi wa nyumba za watumishi 24.
- Ukamilishaji wa zahanati 10.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 49 katika shule za sekondari.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 287 katika shule za msingi.
- Utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kaya 44,760 waliopo katika vijiji/mitaa 512.
- Ujenzi wa ofisi za kata 3.

3.5 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Februari, 2018 mwaka 2017/18 kwa Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ni pamoja na:

- Fedha za miradi kutotolewa kwa wakati.
- Kutolewa fedha kidogo kwa ajili matumizi mengineyo.
- Baadhi ya fedha za miradi kutotolewa.
- Kufutwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato.
- Ukosefu wa soko la mbaazi.
- Kupungua kwa ushuru wa mazao kutoka 5% hadi 3%.
- Kukosekana kwa takwimu sahihi za kukokotoa ushuru wa huduma.

3.6 MAPENDEKEZO

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, Mkoa unapendekeza yafuatayo;-

- Ushuru wa mazao ulipwe kwa kuzingatia bei ya soko ambayo ipo kisheria badala ya bei dira inayotumika katika zao la korosho.
- Tunaiomba Serikali kuingiza mazao mchanganyiko kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani
- Tunaiomba Serikali kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa wakati.
- Tunaiomba Serikali kutoa maelekezo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutoa takwimu sahihi za mapato kwa MSM zinazotokana na watoa huduma/wafanyabiashara katika mamlaka husika.

4.0 MAAGIZO YA KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA

Katika kikao cha kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu 80 Mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2017/2018 kilichofanyika tarehe 30/03/2017 katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliuliza maswali mbalimbali ambayo yalijibiwa wakati wa kikao. Kamati haikutoa maagizo/maazimio mahsusi kwa Mkoa ili kuyatekeleza na kuyatolea taarifa katika kikao kinachofuata.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

4.1 MADUHULI YA MKOA NA MAKUSANYO YA HALMASHAURI.

4.1.1 Makadirio ya maduhuli kwa Sekretarieti ya Mkoa kwa mwaka 2018/19

Katika mwaka 2018/19, Sekretarieti ya Mkoa inakadiria kukusanya maduhuli jumla ya shilingi **4,400,000.00** kutoka vyanzo vya kodi ya pango la mgahawa na ukumbi na uuzaji wa nyaraka za manunuzi kama mapato ya Serikali yanayokwenda moja kwa moja Hazina.

4.1.2 Makadirio na Makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2018/19

Katika mwaka 2018/19, Halmashauri zinakadiria kukusanya mapato ya ndani yenye jumla ya shilingi **28,929,810,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani. Jedwali Na.19 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na.19: Makadirio ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri 2018/19

HALMASHAURI	ENEO		JUMLA
	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	MAKUSANYO LINDWA	
Mtwara Mikindani	4,540,425,000	260,000,000	**4,800,425,000**
Masasi Mji	2,023,552,690	1,094,577,310	**3,118,130,000**
Newala Mji	1,834,602,000	903,450,000	**2,738,052,000**
Nanyamba Mji	1,575,662,000	721,550,000	**2,297,212,000**
Mtwara	2,499,260,000	411,862,000	**2,911,122,000**
Masasi	1,847,681,000	936,488,000	**2,784,169,000**
Nanyumbu	1,813,132,000	1,195,000,000	**3,008,132,000**
Newala	1,102,480,000	703,260,000	**1,805,740,000**
Tandahimba	2,824,014,322	2,642,813,678	**5,466,828,000**
JUMLA	**20,060,809,012**	**8,869,000,988**	**28,929,810,000**

Tanbihi: Orodha ya vyanzo imeoneshwa katika kiambatisho namba 3 kwenye randama.

Fedha zilizotengwa kwa wanawake, vijana na walemavu pamoja na miradi mingine ya maendeleo kutokana na makusanyo yasiyolindwa kwa mwaka 2018/19 ni jumla ya sh. **9,866,747,669.00** ambapo wanawake na vijana (10%) ni sh. **2,006,080,901** na miradi mingine ya maendeleo (30% & 50%) ni sh. **7,860,667,072.** Mchanganuo kwa kila Halmashauri ni kama inavyooneshwa katika jedwali namba 20.

Jedwali Na.20: Matumizi ya Makusanyo Yasiyolindwa katika Miradi -2018/19

HALMASHAURI	MAKUSANYO YASIYOLINDWA	WANAWAKE, VIJANA & WALEMAVU-10%		MIRADI MINGINE-30% & 50%		JUMLA KWA MIRADI YA MAENDELEO-40% & 60%	
		KIASI	%	KIASI	%	KIASI	%
Mtwara MC	4,540,425,000	454,042,500	**10**	2,270,212,500	**50**	2,724,255,000	**60**
Masasi TC	2,023,552,690	202,355,269	**10**	607,065,807	**30**	809,421,076	**40**
Newala TC	1,834,602,000	183,460,200	**10**	550,380,600	**30**	733,840,800	**40**
Nanyamba TC	1,575,662,000	157,566,200	**10**	472,698,600	**30**	630,264,800	**40**
Mtwara	2,499,260,000	249,926,000	**10**	749,778,000	**30**	999,704,000	**40**
Masasi *	1,847,681,000	184,768,100	**10**	923,840,500	**50**	1,108,608,600	**60**
Nanyumbu	1,813,132,000	181,313,200	**10**	543,939,600	**30**	725,252,800	**40**
Newala	1,102,480,000	110,248,000	**10**	330,744,000	**30**	440,992,000	**40**
Tandahimba	2,824,014,322	282,401,432	**10**	1,412,007,161	**50**	1,694,408,593	**60**
JUMLA	**20,060,809,012**	**2,006,080,901**	**10**	**7,860,667,072**	**39**	**9,866,747,669**	**49.18**

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inaomba kuwekwa katika kundi la Halmashauri zinazotakiwa kuchangia 40% ya mapato yake ya ndani kwa miradi ya maendeleo pamoja na mfuko wa wanawake, vijana na walemavu.

4.2 FEDHA ZA RUZUKU KWA MATUMIZI YA KAWAIDA MWAKA 2018/19

Katika mwaka 2018/19 Mkoa unakadiria kukusanya na kutumia fedha za ruzuku toka Serikali kuu jumla ya shilingi **134,316,990,000.00** kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida ambapo Sekretarieti ya Mkoa ni shilingi **7,071,993,000.00 (5.26%)** na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi **127,244,997,000.00 (94.74%).** Kimatumizi fedha hizo zinakusudiwa kugharamia maeneo yafuatayo;

4.2.1 Mishahara – Shilingi 126,444,346,000.00

Katika mwaka 2018/19, kiasi cha shilingi **126,444,346,000.00** kinakadiriwa kutumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi ambapo Sekretarieti ya Mkoa ni shilingi **5,409,810,000.00 (4.28%)** na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi **121,034,536,000.00 (95.72%).**

4.2.2 Matumizi Mengineyo – Shilingi 7,772,643,000.00

Katika mwaka 2018/19, kiasi cha shilingi **7,872,644,000.00** kinakadiriwa kutumika kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo Sekretarieti ya Mkoa shilingi **1,662,183,000.00 (21.11%)** na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi **6,210,461,000.00 (78.89%)**. Mchanganuo wa makadirio ya matumizi ya kawaida kwa fedha za ruzuku mwaka 2018/19, unaonekana katika jedwali namba 21.

Jedwali Na.21: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa ruzuku mwaka 2018/2019.

MAMLAKA	MATUMIZI YA KAWAIDA		
	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA
Sekretarieti ya Mkoa	5,409,810,000	1,662,183,000	**7,071,993,000**
Mamlaka za Serikali za Mitaa			
Mtwara Mikindani	14,306,478,000	656,559,000	14,963,037,000
Masasi Mji	11,372,853,000	540,894,000	11,913,747,000
Newala Mji	8,516,716,000	435,648,000	8,952,364,000
Nanyamba Mji	8,483,060,000	430,055,000	8,913,115,000
Mtwara	12,959,827,000	562,591,000	13,522,418,000
Newala	12,370,979,000	768,338,000	13,139,317,000
Masasi	18,723,391,000	1,039,207,000	19,762,598,000
Tandahimba	19,475,345,000	1,052,568,000	20,527,913,000
Nanyumbu	14,825,887,000	724,601,000	15,550,488,000
Jumla ya MSM	**121,034,536,000**	**6,210,461,000**	**127,244,997,000**
JUMLA KUU	**126,444,346,000**	**7,872,644,000**	**134,316,990,000**

4.2.3 Shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2018/19

Orodha ya baadhi ya shughuli za kawaida zitakazotekelezwa kwa mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo;

a) Sekretarieti ya Mkoa

- Kusimamia ulinzi na usalama katika Mkoa.
- Kuendesha vikao 14 vya kisheria.
- Kulipa mishahara kwa watumishi 483.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi na kuzishauri Halmashauri.
- Kuratibu ziara mbalimbali za viongozi wa kitaifa.
- Kuratibu shughuli za kukimbiza mwenge wa uhuru.

b) Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Kusimamia ulinzi na usalama.
- Kutoa huduma mbalimbali za kila siku kwa wananchi.
- Kukimbiza mwenge wa uhuru.
- Ulipaji wa Mishahara kwa watumishi.
- Kuendesha vikao mbalimbali vya kisheria.

4.3 FEDHA ZA RUZUKU KWA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2018/2019.

Ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/19 Mkoa unakadiria kukusanya na kutumia fedha za ruzuku jumla ya shilingi **48,036,105,500.00** ambapo fedha za ndani ni shilingi **25,252,811,500.00 (52.57%)** na fedha za nje ni shilingi **22,783,294,000.00 (47.43%)**.

Katika fedha hizo Sekretarieti ya Mkoa inakadiria kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi **2,180,942,000.00** ambapo fedha za ndani shilingi **1,730,000,000.00 (79.32%)** na fedha za nje ni shilingi **450,942,000.00 (20.68%)**. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakadiria kukusanya na kutumia jumla ya shilingi **45,855,163,500.00** ambapo fedha za ndani ni shilingi **23,522,811,500.00 (51.30%)** na fedha za nje ni shilingi **22,332,352,000.00 (34.70%)**. Jedwali Na 22 linaonesha mchanganuo wake.

Jedwali Na. 22: Mchanganuo wa fedha za Miradi ya Maendeleo mwaka 2018/19

MAMLAKA	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	JUMLA
Sekretarieti ya Mkoa	1,730,000,000	450,942,000	**2,180,942,000**
Mamalaka za Serikali za Mitaa			
Mtwara Mikindani	2,922,356,500	12,272,393,000	**15,194,749,500**
Masasi Mji	782,827,000	680,078,000	**1,462,905,000**
Nanyamba Mji	4,380,551,500	723,596,000	**5,104,147,500**
Newala Mji	2,984,007,500	527,737,000	**3,511,744,500**
Mtwara	2,466,596,000	921,739,000	**3,388,335,000**
Newala	2,150,414,000	1,000,150,000	**3,150,564,000**
Masasi	3,712,618,500	1,402,706,000	**5,115,324,500**
Tandahimba	1,288,976,500	3,852,923,000	**5,141,899,500**
Nanyumbu	2,834,464,000	951,030,000	**3,785,494,000**
Jumla MSM	**23,522,811,500**	**22,332,352,000**	**45,855,163,500**
JUMLA	**25,252,811,500**	**22,783,294,000**	**48,036,105,500**

4.3.1 Miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2018/19

Orodha ya baadhi ya programu/miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2018/19 ni pamoja na;

a) Sekretarieti ya Mkoa

- Ukarabati wa jengo la ofisi ya mkuu wa mkoa.
- Ujenzi wa ofisi 3 za tarafa.
- Ujenzi wa kituo bora cha elimu.
- Usimamizi wa programu ya maji vijijini na usafi wa mazingira.
- Ujenzi wa nyumba 3 za Maafisa Tarafa.
- Utekelezaji wa mfuko wa pamoja wa sekta ya afya.
- Utekelezaji wa program ya usimamizi wa fedha za umma.
- Ukarabati wa ofisi za 5 za wakuu wa wilaya.
- Ujenzi wa nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa.

b) Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Ujenzi wa miradi 73 ya maji.
- Ujenzi wa vituo vya afya 3.
- Utekelezaji wa shughuli za mfuko wa jimbo.
- Utoaji wa elimu bila malipo katika shule zote za msingi na sekondari.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 136 kwa shule za msingi.
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa 78 kwa shule za sekondari.
- Ujenzi wa majengo manne (2) ya utawala kwa Halmashauri za Newala Mji na Nanyamba Mji.
- Ujenzi wa nyumba za watumishi 70.
- Ukamilishaji wa zahanati 10.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 212 katika shule za sekondari kati ya 598 yanayotakiwa.
- Ujenzi wa matundu ya vyoo 612 katika shule za msingi kati ya 6,744 yanayotakiwa.
- Utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kaya 44,760 waliopo katika vijiji/mitaa 512.
- Ujenzi wa ofisi za kata 7.
- Kuanza ujenzi wa hospitali 3 kwa Halmashauri 3 (Masasi, Nanyamba Mji na Mtwara)

5.0 HITIMISHO

Jumla ya fedha zinazokadiriwa kukusanywa na kutumika na Mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2018/2019 ni shilingi **208,626,274,500.00**. Kati ya fedha hizo ***Mishahara*** ni shilingi **126,444,346,000.00** sawa na **59.75%**, ***Matumizi ya Mengineyo*** ni shilingi **22,518,351,000.00** sawa na **10.64%** na ***Miradi ya Maendeleo*** shilingi **59,663,577,500.00** sawa na **29.61%.** Jedwali Na. 23 linaonesha mchanganuo huo.

Jedwali Na.23: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mkoa mwaka 2018/2019

MAMLAKA	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	MIRADI YA MAENDELEO	
			FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE
RS	5,409,810,000	1,662,183,000	1,730,000,000	450,942,000
HALMASHAURI	121,034,536,000	20,856,168,000	35,150,283,500	22,332,352,000
JUMLA	**126,444,346,000**	**22,518,351,000**	**36,880,283,500**	**22,783,294,000**
	148,962,697,000		**59,663,577,500**	
JUMLA KUU	**208,626,274,500**			

Hivyo, kwa jumla naomba kuidhinishiwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mkoa wa Mtwara (Fungu 80) jumla ya shilingi **208,626,274,500.00** kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Naomba kuwasilisha,

Gelasius G. Byakanwa
MKUU WA MKOA
MTWARA